**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA YA MHESHIMIWA JAJI WA RUFAA JACOBS C. M. MWAMBEGELE MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI KWA UMMA KUHUSU KUGAWA AU KUBADILI MAJINA YA MAJIMBO YA UCHAGUZI KWA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

***Ndugu waandishi wa habari!***

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 10(1)(d) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka na jukumu la kuchunguza, kupitia mipaka na kugawa majimbo ya uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano.

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 18(1) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, kupitia vyombo vya habari, Tume ilitoa tangazo kuutaarifu umma kuhusu kuanza kwa mchakato wa kugawa au kubadili majina ya majimbo ya uchaguzi kuanzia tarehe 27 Februari hadi 26 Machi, 2025.

Tangazo hilo liliweka utaratibu na vigezo vitakavyozingatiwa na Tume wakati wa kugawa au kubadili majina ya majimbo ya uchaguzi. Kufuatia tangazo hilo Tume ilipokea jumla ya maombi thelathini na nne (34) ya kugawa majimbo ya uchaguzi na maombi kumi (10) ya kubadili majina ya majimbo.

***Ndugu waandishi wa habari!***

Baada ya kupokea maombi na kwa kuzingatia kanuni ya 18 (5) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume ilitembelea na kufanya vikao na wadau katika baadhi ya majimbo yaliyoomba kugawanywa pamoja na majimbo yote

yaliyoomba kubadilishwa majina ili kujiridhisha na taarifa za maombi zilizowasilishwa Tume.

Leo tarehe 12 Mei, 2025 tumewaita ili tuwatangazie majimbo mapya yaliyogawanywa, majimbo yaliyobadilishwa majina, idadi ya majimbo yote kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge na idadi ya kata zote kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

## 2.0 MAJIMBO MAPYA YA UCHAGUZI YALIYOANZISHWA

***Ndugu waandishi wa habari!***

Pamoja na vigezo vya ugawaji wa majimbo vilivyoainishwa, Tume imezingatia zaidi vigezo vinne ambavyo imevipa uzito kwenye mchakato wa ugawaji wa majimbo. Vigezo hivyo ni:-

a. idadi ya watu, ambapo kwa majimbo ya mjini kigezo kilikuwa kuanzia watu 600,000 na kwa majimbo ya vijijini ilikuwa kuanzia watu 400,000;

b. uwezo wa ukumbi wa Bunge; kwamba kwa sasa ukumbi wa Bunge una uwezo wa kuchukua wabunge wapya wangapi;

c. idadi ya wabunge wanawake wa viti maalum; na

d. jimbo moja la uchaguzi kutokuwa katika wilaya au halmashauri mbili.

Kwa kuzingatia vigezo hivyo na masharti ya ibara ya 75(1), (2) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kanuni ya 18(7) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, baada ya kuchakata maombi husika, Tume imekubali na kuanzisha majimbo mapya nane (08) yafuatayo:

**a. Mkoa wa Dar es Salaam** yameanzishwa majimbo mawili kama ifuatavyo:-

i. Jimbo la Uchaguzi la **UKONGA** limegawanywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **KIVULE**; na

ii. Jimbo la Uchaguzi la **MBAGALA** limegawanywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **CHAMAZI.**

b. **Mkoa wa Dodoma** limeanzishwa jimbo jipya moja, ambapo Jimbo la Uchaguzi la **DODOMA MJINI** limegawanywa na kuanzishwa jimbo jipya la Uchaguzi la **MTUMBA.**

c. **Mkoa wa Mbeya** limeanzishwa jimbo jipya moja, ambapo Jimbo la Uchaguzi la **MBEYA MJINI** limegawanywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **UYOLE.**

d. **Mkoa wa Simiyu** limeanzishwa jimbo jipya moja. Ambapo Jimbo la Uchaguzi la **BARIADI** limegawanywa na kuanzishwa jimbo jipya la uchaguzi la **BARIADI MJINI.**

e. **Mkoa wa Geita** yameanzishwa majimbo mawili kama ifuatavyo:-

   i. Jimbo la Uchaguzi la **BUSANDA** limewaganywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **KATORO;** na

   ii. Jimbo la Uchaguzi la **CHATO** limegawanywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **CHATO KUSINI.**

f. **Mkoa wa Shinyanga** limeanzishwa jimbo jipya moja, ambapo Jimbo la Uchaguzi la **SOLWA** limegawanywa na kuanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la **ITWANGI.**

## 3.0 MAJIMBO YA UCHAGUZI YALIYOBADILISHWA MAJINA

***Ndugu waandishi wa habari!***

Tume imebadili majina ya majimbo ya uchaguzi kumi na mbili (12) kama ifuatavyo: -

a. **Mkoa wa Geita,** Halmashauri ya Wilaya ya Chato: Baada ya kugawanywa Jimbo la **CHATO** na kuanzisha Jimbo jipya la uchaguzi la **CHATO KUSINI.** Jimbo la sasa la **CHATO** limebadilishwa jina, litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **CHATO KASKAZINI.**

b. **Mkoa wa Kagera, Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi:** Jimbo la Uchaguzi la **NKENGE** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **MISSENYI.**

c. **Mkoa wa Katavi, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika:** Jimbo la Uchaguzi la **MPANDA VIJIJINI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **TANGANYIKA.**

d. **Mkoa wa Kigoma, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko:** Jimbo la Uchaguzi la **BUYUNGU** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **KAKONKO.**

e. **Mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Bariadi:** Baada Jimbo la **BARIADI** kugawanywa na kuanzisha Jimbo jipya la uchaguzi la **BARIADI MJINI.** Jimbo la sasa la **BARIADI** limebadilishwa jina, litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **BARIADI VIJIJINI.**

f. **Mkoa wa Singida,** majimbo matano yamebadilishwa majina kama ifuatavyo:-

   i. **Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni:** Jimbo la Uchaguzi la **MANYONI MASHARIKI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **MANYONI**

   ii. **Halmashauri ya Wilaya ya Singida:** Jimbo la Uchaguzi la **SINGIDA KASIKAZINI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **ILONGERO.**

   iii. **Halmashauri ya Wilaya ya Itigi:** Jimbo la Uchaguzi la **MANYONI MAGHARIBI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **ITIGI**

   iv. **Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi:** Jimbo la Uchaguzi la **SINGIDA MASHARIKI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **IKUNGI MASHARIKI**

   v. **Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi:** Jimbo la Uchaguzi la **SINGIDA MAGHARIBI** limebadilishwa jina, sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **IKUNGI MAGHARIBI**

g. **Mkoa wa Tabora, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui:** Jimbo la Uchaguzi la **Tabora Kaskazini** limebadilishwa jina sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **UYUI; na**

h. **Mkoa wa Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Vijijini:** Jimbo la Uchaguzi la **HANDENI VIJIJINI** limebadilishwa jina sasa litaitwa Jimbo la Uchaguzi la **HANDENI.**

## 4.0 IDADI YA MAJIMBO YA UCHAGUZI

***Ndugu waandishi wa habari!***

Kutokana na kuongezeka kwa majimbo mapya ya uchaguzi nane (08) kama nilivyoeleza awali, napenda kuwatangazia kuwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 jumla ya majimbo ya uchaguzi 272 yatatumika kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge, katika Jamhuri ya Muungano. Kati ya majimbo hayo, 222 yapo Tanzania Bara na majimbo 50 yapo Tanzania Zanzibar. Orodha ya majimbo yote itachapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

## 5.0 IDADI YA KATA ZA UCHAGUZI

***Ndugu waandishi wa habari!***

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 5(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, napenda kutangaza rasmi kwamba, jumla ya kata 3,960 zitatumika kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani kwa Tanzania Bara katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Kata hizo 3,960 ni ongezeko la kata mpya tano (05) za Ngereyani na Sinonik katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido na kata za Mupi, Bwawani Mjini na Shela katika Halmashauri ya Mji Rufiji ambazo zilianzishwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Orodha ya kata zote za Tanzania Bara itachapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

## 6.0 HITIMISHO

***Ndugu waandishi wa habari!***

Napenda kutumia fursa hii kuwataarifu wananchi kuzingatia mabadiliko haya ya maeneo ya uchaguzi ili waweze kutumia haki yao ya msingi ya kushiriki kugombea na kupiga kura siku ya kupiga kura.

*Ndugu waandishi wa habari!!*

Mwisho, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika awamu ya pili kwa mikoa kumi na sita (16) iliyobakia, kuhakiki taarifa zao katika Daftari la Awali la Wapiga Kura linalowekwa wazi katika kila kituo na kujiandaa vyema kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza

Jaji (Rufaa) Jacobs C. M. Mwambegele
**MWENYEKITI**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**
**12 Mei, 2025**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

# ORODHA YA MAJIMBO YALIYOGAWANYWA NA MAJIMBO MAPYA

| Na. | MKOA | Halmashauri | Jimbo lililopo | Na. | Jimbo Jipya lililoanzishwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar Es Salaam | Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam | Ukonga | 1. | Jimbo la Kivule |
| | | Halmashauri ya Manispaa Temeke | Mbagala | 2. | Jimbo la Chamazi |
| 2. | Dodoma | Halmashauri ya Jiji la Dodoma | Dodoma Mjini | 3. | Jimbo la Mtumba |
| 3. | Mbeya | Halmashauri ya Jiji la Mbeya | Mbeya Mjini | 4. | Jimbo la Uyole |
| 4. | Simiyu | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi | Bariadi Vijijini | 5. | Bariadi Mjini |
| 5. | Geita | Halmashauri ya Wilaya ya Geita | Busanda | 6. | Katoro |
| | | Wilaya ya Chato | Chato Kaskazini | 7. | Jimbo la Chato Kusini |
| 6. | Shinyanga | Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga | Solwa | 8. | Itwangi |

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

# MAJIMBO YALIYOBADILISHWA MAJINA

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Jina la awali la Jimbo | Jina jipya la Jimbo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kagera | Wilaya ya Misenyi | Nkenge | Misenyi |
| 2. | Katavi | Wilaya ya Tanganyika | Mpanda Vijijini | Tanganyika |
| 3. | Kigoma | Wilaya ya Kakonko | Buyungu | Kakonko |
| 4. | Singida | Wilaya ya Manyoni | Manyoni Mashariki | Manyoni |
| 5. | Singida | Wilaya ya Singida | Singida Kaskazini | Ilongero |
| 6. | Singida | Wilaya ya Itigi | Manyoni Magharibi | Itigi |
| 7. | Singida | Wilaya ya Ikungi | Singida Mashariki | Ikungi Mashariki |
| 8. | Singida | Wilaya ya Ikungi | Singida Magharibi | Ikungi Magharibi |
| 9. | Tabora | Wilaya ya Uyui | Tabora Kaskazini | Uyui |
| 10. | Tanga | Wilaya ya Handeni | Handeni Vijijini | Handeni |
| 11. | Geita | Wilaya ya Geita | Chato | Chato Kaskazini |
| 12. | Simiyu | Wilaya ya Bariadi | Bariadi | Bariadi Vijijini |